TANGAZO LA SERIKALI Na. 582 la tarehe 12/7/2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya Kifungu cha 7(1) na 16 (1))*

## SHERIA NDOGO YA USHURU WA ZAO LA MKONGE YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA YA MWAKA 2024

Jina na kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ushuru wa Zao la Mkonge ya Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii isipokuwa kama mktadha utahitaji vinginevyo-

"afisa mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi baada ya kushauriana na Bodi ya Mkonge kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

Sura ya 55

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Mkonge Tanzania iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Mkonge;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga;

Suar ya 212

"kampuni" maana yake ni kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Kampuni;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi chini ya Sheria Ndogo hii;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

"Mkonge" maana yake ni majani au singa au nyuzi zitokanazo na mmea wa Mkonge;

"mlipa ushuru" maana yake ni mtu au kampun, tawi la kampuni au kikundi cha watu kinachofanya shughuli za ununuzi wa mkonge katika eneo la Halmashauri;

"Ushuru" maana yake ni tozo ya mazao ya Mkonge ya asilimia tatu ya bei ya mauzo;

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi au kikundi cha watu, Kampuni au Shirika, ambalo limeteuliwa na Halmashauri kufanya kazi yoyote chini ya Sheria Ndogo hii kwa niaba ya Halmashauri.

Utozaji wa ushuru

4. Halmashauri itatoza ushuru wa zao la Mkonge kwa kiwango cha asilimia tatu ya bei ya mauzo kutoka kwa kila mnunuzi wa zao hilo kwenye eneo la Halmashauri.

Mgawanyo wa mapato

5. Katika kutekeleza majukumu ya pamoja kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, asilimia tatu ya ushuru iliyorejewa katika kanuni ya 4 itagawanywa kama ifuatavyo-

(a) Halmashauri asilimia mbili;
(b) Bodi ya Mkonge Tanzania asilimia sifuri nukta tano;
(c) Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) asilimia sifuri nukta mbili tano; na
(d) Taasisi ya Mafunzo ya Kilimo iliyo chini ya Wizara ya Kilimo (MATI) iliyopo Mlingano Mheza asilimia sifuri nukta mbili tano.

Usafirishaji wa Mkonge

6.-(1) Mtu yeyote hataruhusiwa kusafirisha Mkonge kutoka nje ya eneo la Halmashauri bila kuwa na kibali kutoka kwa Halmashauri.

(2) Mtu yeyote anayetaka kusafirisha Mkonge atatakiwa kuomba kibali kwa njia ya maandishi.

(3) Halmashauri itatoa kibali cha kusafirisha Mkonge kwa mwombaji ndani ya siku saba toka tarehe

ya maombi kuwasilishwa na kupokelewa na Halmashauri.

Wajibu wa mnunuzi

7. Kila mnunuzi atakuwa na wajibu wa-
(a) kulipa ushuru wa asilimia tatu ya bei ya mauzo kwa Halmashauri au wakala wake;
(b) kupokea stakabadhi ya kielektoniki ya malipo ya ushuru kutoka kwa Halmashauri au wakala wake;
(c) kuomba kibali cha kusafirisha Mkonge kwenda nje ya eneo la Halmashauri; na
(d) kuomba kibali cha kununua Mkonge katika eneo la Halmashauri.

Uwezo wa kukagua na Kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo

8. Kwa madhumuni ya usimamizi wa Sheria Ndogo hii, afisa mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika eneo lolote ndani ya Halmashauri kwa ajili ya-
(a) kukagua kumbukumbu na taarifa zinazohusu shughuli za mauzo ya Mkonge kwa lengo la kutambua kiasi ambacho mlipa ushuru anastahili kulipa; na
(b) kukagua na kujiridhisha kama kiasi cha Mkonge kilichokatiwa kibali cha kusafirishwa nje ya Halmashauri kiko sawa au kinalingana na kiasi halisi kinachosafirishwa.

Makosa na adhabu

9.-(1) Mtu yeyote atakuwa anatenda kosa endapo-
(a) atamzuia au atajaribu kumzuia Mkurugenzi au afisa mwidhiniwa kutekeleza wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hii;
(b) atamshawishi mtu mwingine kumzuia Mkurugenzi au afisa mwidhiniwa kutekeleza wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hii;
(c) atasafirisha zao la Mkonge kwenda nje ya eneo la Halmashauri bila ya kibali;
(d) atajihusisha na biashara ya Mkonge bila kuwa na kibali cha ununuzi wa Mkonge

kinachotolewa na Halmashauri;

(e) atakwepa au kushindwa kulipa ushuru wa zao la mkonge chini ya Sheria Ndogo hii;

(f) atamshawishi mlipa Ushuru kukataa au kukwepa kulipa Ushuru; au

(g) atakataa bila sababu za msingi kutoa taarifa zinazohitajika kwa Mkurugenzi au afisa mwidhiniwa zinazohusu ushuru wa zao la Mkonge; au

(h) atawasilisha kwa Halmashauri taarifa zisizo sahihi;

(2) Mtu yeyote atakayetiwa hatiani kwa kutenda kosa chini ya kifungu kidogo cha (1) atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote.

Ufifilishaji wa kosa

10.-(1) Bila kujali masharti ya Sheria Ndogo hii kuhusiana na adhabu, Mkurugenzi anaweza kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu atakaye kiri kutenda kosa kiasi cha Shilingi laki moja.

(2) mtu atakaye kiri kosa chini ya kanuni ndogo ya (1) atajaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 10 (2))*

FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ……………………………………………………………………..……. mwenye Simu Na.………………………………..... wa S.L.P………….………………………………..ninayefanya biashara……………………………….. katika eneo la ……………………….. lililopo katika eneo la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga, kwa hiari yangu mwenyewe nakiri kuwa tarehe………mwezi………… Mwaka…………. nilikiuka masharti ya kanuni ya………… ya Sheria Ndogo ya Ushuru wa Zao la Mkonge ya Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga ya mwaka 2024.
Kwa hiyo, kwa hiari yangu mwenyewe na bila kushurutishwa na mtu yeyote nakubali kulipa kiasi cha shilingi laki moja badala ya kushtakiwa Mahakamani na nipo tayari kutimiza wajibu wangu kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Nathibitisha kwamba maelezo hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa mimi mwenyewe kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu
Jina………………………………………………………………….
Saini: …………………………Tarehe: ……………………………

MBELE YANGU:
Jina: …………………………………………………………………
Saini: ……………………………………………………………….
Wadhifa: ……………………………………………………………
Tarehe: ………………………………………………………………

*Tangazo la Serikali Na.582 (Linaendelea.)*

Muhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga ulibandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio la Mkutano wa Baraza la Halmashauri ya Wilaya ulioitishwa na kufanyika tarehe 1/3/2023 na muhuri wa Halmashauri ilibandikwa mbele ya:-

MWAJUMA A. NASOMBE,
*Mkurugenzi mtendaji,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Mwanga*

MHE. Dr. SALEHE R. MKWIZU,
Mwenyekiti,
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Mwanga*

L.S

**NAKUBALI**,

Dodoma,
30 Januari, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
WAZIRI wa NCHI OR-TAMISEMI,